# CLASS 8 MID TERM 2 OCTOBER 2020

# KISWAHILI

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa**

Katika gazeti moja __1__ ,habari __2__ vichwa vya habari ni za wanafunzi wanaojiunga na shule za upili .Kuna kijana mmoja kutoka kaunti ya Baringo ambaye wazazi wake hawangeweza kumlipia __3__. Habari zake zilipotangazwa wahisani walijitokeza __4__ . Nadai kuwa ni jambo la __5__ kuona kuwa baadhi ya wanafunzi waliofuzu mwaka jana katika mtihani wa K.C.P.E, asilimia kubwa yao __6__ na kidato cha kwanza. Hali hii __7__ tu na ukosefu wa karo bali pia misimamo hasi katika jamii zetu. Tumewaona wasichana wakigeuzwa __8__ na kutumiwa kama chambo cha kunasia utajiri kwa __9__ mapema..

1. A. humu nchini mwetu B. hapa nchini yetu C. hapa nchini mwetu D. huku nchini mwetu
2. A. iliyogonga B. zilizogonga C. zilipogonga D. ilipogonga
3. A. karo B. koto C. fola D. kiingilio
4. A. kumdhamini masomo yake B. kumthamini masomo yake C. kuyadhamini masomo yake D. kuidhamini masomo yake
5. A. kutia moyo B. kufuja moyo C. kuvunja moyo D. kushika kani
6. A. hawatajiunga B. haitajiunga C. hawajiungi D. hawashiriki
7. A. haisababishwi B. haisababishi C. inasababishwa D. ninasababisha
8. A. watwana B. yaya C. wawili D. wajakazi
9. A. kuoa B. kuolea C. kuozwa D. kuoleka

Sijali __10__ mahakamani kwa tuhuma za kumpiga risasi mwenzake. Aliposimamishwa __11__, ushuhuda ulitolewa __12__. Mwishowe ilibainika kuwa alifanya kosa __13__ kimakusudi . Naam, __14__ . Hakimu __15__ hiyo na kumfunga kifungo cha miaka kumi na sita.

10. A. alifika B. alifikwa C. alifikia D. alifikishwa
11. A. rumande B. jela C. kizimbani D. kortini
12. A. juu yake B. dhidi yake C. chini yake D. kando yake
13. A. hiyo B. huo C. hicho D. hilo
14. A. msiba wa kujitakia hauna kilio B. bahari haivukwi kwa kuogelea C. maskini na mwanawe tajiri na mali yake D masukuzi ya leo ndio msitu wa kesho
15. A. aliahirisha kesi B. alikata kesi C. alifuta kesi D. alifungua kesi



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi***

16. **Andika kwa wingi :**
Baraza langu huongozwa na nahodha bahili
A. Mabaraza yetu huongozwa na manahodha bahili
B. Baraza zetu huongozwa na manahodha mabahili
C. Mabaraza yangu huongozwa na nahodha bahili
D. Mabaraza yetu huongozwa na manahodha mabahili

17. **Kanusha:**
Nguo ambayo ilinunuliwa ilivutia sana
A. Nguo ambayo haikununuliwa haivutii sana
B. Nguo ambayo haijanùnuliwa inavutia sana
C. Nguo isiyonunuliwa haivutii sana
D. Nguo ambayo ilinunuliwa haikuvutia sana

18. Chagua sentensi mwafaka inayounganisha hizi
(i) Kikataa kilipata mbolea ya kutosha
(ii) Kikataa hakikutoa mazao ya kutosha
A. Lau kikataa kilipata mbolea hakikutoa mazao ya kutosha
B. Kikataa kilipata mbolea ya kutosha aghalabu hakikutoa mazao ya kutosha
C. Licha ya kikataa kupata mbolea ya kutosha hakikutoa mazao ya kutosha
D. Madhali kikataa kilipata mbolea ya kutosha, hakikutoa mazao ya kutosha

19. Chagua sentensi yenye kiashiria cha karibu
A. Mawaidha haya ninayokueleza yahifadhi moyoni
B. Karibu na nyumba ile kùna jengo jingine
C. Mitungi hiyo aliyobeba haina maji
D. Taifa huru halipaswi kuwa na ufisadi.

20. Chagua sentensi yenye vielezi vya namna
A. Ndege huyo ametua mtini
B. Alifeli swali lenyewe ilhali alifunzwa jana
C. Nilikaa kimya na kusikiliza kwa makini
D. Motokaa hiyo ilipita pale jana

21. Chagua sentensi yenye nomino, kivumishi, kitenzi na kielezi mtawalia.
A. Wanafunzi aghalabu huondoka jioni
B. Alipofika kwao alikuwa amechoka
C. Kitabu hicho kina jalada zuri
D. Mwalimu huyo alitusaidia sana

22. **Chagua jibu sahihi**
A. Kikuba ni pambo la shingoni
B. Ndonya huvaliwa kiunoni
C. Jina jingine la kipuli ni kipini
D. Furungu huvaliwa masikioni na miguuni

23. Chagua sentensi ambayo ina matumizi ya kiambishi <u>- ki-</u> cha wakati pekee
A. Mwalimu akinipongeza nitafurahi sana
B. Mwalimu alipofika shuleni alimkuta akisoma
C. Chumba hiki kimepambwa vyema
D. Mjomba wangu hupenda kuvaa kizamani

24. **Badilisha sentensi hii katika kauli ya kutendwa**
Jaji amemfunga babu kwa miaka ishirini
A. Jaji amefungwa na babu kwa miaka ishirini
B. Babu amefungiwa na jaji kwa miaka ishirini
C. Jaji amefungia babu kwa miaka ishirini
D. Babu amefungwa na jaji kwa miaka ishirini

25. **Tegua kitendawili kifuatacho:**
Babu akipiga mbizi huibuka na ndevu nyeupe
A. muwa B. mwiko
C. mbegu D. mahindi

26. **Bainisha kiwakilishi katika sentensi ifuatayo:**
Hawa wanapinga vikali ufisadi
A. hawa B. vikali
C. wanapinga D. ufisadi

27. **Sentensi hii imetumia tamathali gani za lugha?**
Mwalimu wetu ni kamusi. Anatema maneno kama mjuzi mwenyewe
A methali, sitiari B. nahau, tashbihi
C. tashbihi, istiara D. istiara, tashbihi

28. Kipi ni kivumishi kilichoundwa kutokana na nomino
A. Pika — mpishi B. onea — onevu
C. Kicheko — mcheshi D. Dhaifu — dhoofu

29. Ni sentensi gani yenye - na- ya kuonyesha mtendaji ?
A. Mwanafunzi na mwalimu huelewana vyema
B. Amekaa karibu na ukuta
C. Mimea katika shamba imeharibiwa na ndovu
D. Wazazi wana matumaini kwa watoto wao

30. Mhudumu wa ofisini anayetunza nyaraka na majadala ni ?
A. Katikiro B. Kaimu
C. Mhazili D. Mshenga

31. Ila ya Pondamali ilikuwa,
A. alipenda sana kujumuika na marafiki zake katika magenge ya burudani
B. alipenda bibi yake asalie nyumbani yeye akienda katika burudani zake
C. kutoweza kujua ni wakati gani alipaswa kuwa nyumbani
D. kutokuwa na watu wengine wa kumsaidia wakati wa shida

32. Ni wazi kuwa
A. Pondamali alithamini sana starehe kuliko masuala muhimu ya kinyumbani
B. marafiki wabaya ndio waliomfunza Pondamali tabia ya kunywa pombe
C. Pondamali alikuwa mkunga shupavu ndiyo maana bibi yake alitaka abaki nyumbani
D. Pondamali alikuwa mtu aliyethamini jamii na matendo ongofu

33. Kwa mujibu wa kifungu ulichosoma,
A. Pondamali ndiye alimtafutia bibi yake marafiki pale mtaani
B. Pondamali ndiye alikuwa na marafiki wengi pale mtaani kuliko bibi yake
C. Pondamali ndiye alikuwa kipenzi cha wengi pale mtaani kuliko bibi yake
D. Pondamali ndiye aliyesababisha hali ya upweke wa bibi yake

34. Pesa za Pondamali zilipoisha akiwa katika starehe zake,
A. aliamua kukopa pombe ili kukidhi kiu yake
B. alianza kuzua fujo
C. aliamua kurudi nyumbani
D. alipiga simu ili kuletewa pesa zaidi

35. Ukweli <u>halisi</u> ni kuwa
A. mkewe Pondamali hakuwa akipendezwa na uraibu wa bwanake
B. mkewe Pondamali alijua siku moja angekufa kutokana na tabia za mumewe
C. Pondamali alitiwa motisha wa ulevi na bibi yake
D. Hapana mtu mwingine aliyejua ulevi wa Pondamali isipokuwa mkewe

36. Kifunguamimba ni ________
A. mtoto wa mwisho kuzaliwa
B. ndugu anayemfuata mwingine
C. mtoto wa katikati
D. mtoto wa kwanza kuzaliwa

37. Methali ondoa dari ezeka paa inadhihirika pale
A. Pondamali anapata pesa za mafuta taa na kukosa za ulevi
B. Pondamali anapata pesa za ulevi na kukosa za mafuta taa
C. Pondamali anapokosa kumsaidia mkewe kujifungua
D. Pondamali anarudi kwake wakati wa giza totoro

38. **<u>Mkewe alikuwa mtu wa kuzungumza na kimya chake hicho kilikuwa na sababu</u>**. Ni methali gani inayoafiki kauli hii ?
A. Mke ni nguo mgomba kupalilia
B. Kimya kingi kina mshindo mkuu
C. Ndovu akitamba ni masika
D. Ndovu halemewi na mwiro wake

39. Ni wazi kuwa
A. Pondamali hakujutia kitendo chake
B. Pondamali angeendelea na starehe zake
C. Pondamali alijutia ulevi wake
D. Pondamali alijivunia ulevi wake

40. Ni nini maana ya ***'aliyemhiliki'*** ?
A. Aliyemwuuguza B. Aliyemdhuru
C. Aliyemharibu D. Aliyemwangamiza

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50</u>**

Duniani tuko na michezo ya aina nyingi sana. **<u>Tuko na mwajificho, tuko na kushikana na kuangushana,</u>** soka na riadha. Hata hivyo umaarufu wa michezo hii ni tofauti. Kuna ile yenye umaarufu mkubwa na kuna mingine ambayo umaarufu wake ni mdogo.

Mchezo wa soka huwavutia watu wengi sana. Mashabiki wanaweza kujinyima kila kitu ili watazame mchezo runingani. Ule unaovutia zaidi ni wa kombe la dunia. Watu hujipanga na kuwa mashabiki wa timu fulani, kiasi kwamba wanaweza kupigana. Unaweza kufikiria wale wanaocheza ni ndugu zao au wazazi wao. Wengine huwekeana kinyongo badala ya kushabikia pamoja. Kuna wengine wanawekeana ahadi fulani kwamba timu yake ikishinda atapenda kitu fulani na wakati mwingine kitu hicho huwa ni pesa. Ajabu ni kwamba, wale wanaowekeana ahadi hawachezi. Ni watazamaji tu.

Tumeshuhudia misukosuko ikizuka hasa katika familia watu wakiunga mkono upande fulani. Baba anaweza kuwa upande mmoja, mama mwingine na watoto mwingine. Shida ni bao likifungwa .Wengine wakishangilia wenzao huwa wanasononeka. Iwapo kushangilia hakutadhibitiwa ipasavyo, basi mzozo unaweza kutokea. Wasioshangilia huona kama kwamba wanadharauliwa . Kushangilia kwa mama kunaweza kumletea talaka ambayo hakuilalia wala kuiamkia. Hapa ndipo busara ya asiyekubali kushindwa si mshindani inafaa kuangaziwa.


Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40**

Mzee Pondamali alikuwa amethamini sana starehe. Mara nyingi ni zile ungempata katika vituo vya burudani. Kasoro yake ilikuwa hakuweza kutofautisha nyakati za dharura ili abaki nyumbani. Kuna wakati bibi yake alikuwa mjamzito na angejifungua wakati wowote. Alipomwona Pondamali akitoka , alimwomba kubaki naye lakini yote yaliangukia masikio yaliyotiwa nta. Bwana Pondamali alisema, " Nani huyo amekuambia kuwa utajifungua leo usiku? Hata hujui ulihimili lini ?"

Siku za mwisho wa mwezi huwa na shughuli nyingi. Wengi huwa na mishahara mfukoni. Vivyo hivyo Bwana Pondamali pia alikuwa na mshahara wake mfukoni. Basi angewezaje kubaki na bibi yake ilhali wenzake walikuwa magengeni wakimsubiri ? Usisahau ahali wake alikuwa tayari kujifungua **kifunguamimba.** Mkewe hakuwa na ndugu wala rafiki wa kumsaidia. Kijijini kwao hakuwa na yeyote isipokuwa mavyaa. Vilevile Pondamali alimkataza kushirikiana na yeyote pale kariani.

Usiku huo , Pondamali alitoka na kusindika mlango nyuma kwa kishindo . Alitokomea na kutoweka gizani kama umande unavyotoweka jua linapochomoza. Akazama juu na kwenda kujiunga na wenzake katika starehe za mbwa kukalia mkia wake.

Kufikia usiku wa manane, fedha zikawa zimemkatikia. Basi akawa hana lingine ila kuelekea nyumbani huku akijikokota kwa ulevi. Begani alikuwa amejitwika kiatu kimoja kwenye mkono wa kushoto na shati lake lililowa jasho kwa joto la ile pombe aliyoinywa kwa mkono wa pili. Kila alipopita aliacha uvundo wa pombe nyuma yake . Pondamali alikuwa na mazoea ya kufungua mlango wa nyumba yao kwa teke moja hafifu kila alipofika usiku wa manane akiwa chopi. Baada ya kudai chakula alijibwaga kitandani kama gunia la makopa na kuanza kukoroma mfululizo kama chura. Mkewe kuona hivi alikuwa akimwambia "usipowacha kulewa namna hii siku moja utajiuma kidole."

Nyumbani kwake aliporejea giza lilikuwa limesheheni kote. Baada ya kufungua mlango kwa teke, alimwita mkewe kwa ukali.Alijibiwa na kimya cha makaburini. "Je, anaweza kuwa wapi mwanamke huyu usiku huu ?" Akiyumbayumba kama dau katika tufani kali, alichomoa kiberiti chake mfukoni na kukiwasha kibatari kilichokuwa mezani. Lakini hakikuwaka. Hakikuwa na hata tone la mafuta taa. Alipepesuka na kuelekea hadi kitandani. Kilikuwa kitupu. Shuka chafu kuukuu ndizo zilikuwa zimerudikwa ovyo.

Hapo Pondamali alianza kupandwa na madadi huku akimwita ahali wake kwa ghamidha. Hata hivyo alichokisikia ni mwangwi wake mwenyewe. Nje kila kitu kilitulia tuli na upepo nao ulikuwa shwari. Mwezi nao ulikuwa umeanza kujitokeza nyuma ya mawingu meusi yaliyokuwa yakipita kwa kasi angani. Polepole miale ya mbalamwezi ilianza kupenyeza kupitia kwenye dirisha lililokuwa limefunguliwa nusu. Pondamali alirudi nyuma na kuchungulia chumbani kwa makini.

Hapo ndipo alimwona mkewe amelala yombo kama bahasha. Alikuwa ametulia tuli kama maji ya mtungi. Pondamali alishangazwa na ukimya uliotanda chumbani. **Mkewe alikuwa mtu wakuzungumza na kimya chake hicho, kilikuwa na sababu**. Pondamali aliinama huku akipumua kwa nguvu na kuteuka kwa kwikwikwi. Hapo aliunyanyua mkono wa mkewe. Ulikuwa baridi kuliko barafu. Pondamali alipiga magoti na kuyaangalia macho ya mkewe. Yalikuwa yametoka nje yaking'aa kama glasi iliyoingiwa na umande. Uso wake ulikuwa umegeuka rangi ya kijivu na kinywa kilikuwa wazi.

Hapo Pondamali akapiga ukemi uliowaita wa mbali na wa karibu. Nao majirani walifika wakiwa wamejihami kwa zana hatari za vita. Wakati huu Pondamali alikuwa ameleuka . Alianza kumsukasuka mkewe kwa nguvu na kujaribu kumwamsha. Kumbe alipokuwa akijiburudisha na wenzake , mkewe alishikwa na uchungu wa kujifungua .Ikawa vigumu hata kutoka kitandani .Alijikokota hadi kizingitini alipolemewa na kukata roho. "Usipowacha kulewa namna hii, siku moja utajiuma kidole ." Hapo akaona ni yeye **aliyehiliki** mke wake.?

Ni jambo la kushangaza kuona watu wazima wakikosana kwa sababu ya ngozi iliyowambwa na kutiwa upepo ndani .Wachezaji hufanya hivyo kwa sababu wanatarajia pato. Lakini mashabiki hufanya hivyo kwa sababu gani ? Kwangu binafsi siuonei fahari mchezo huu kwa kuwa wengi wanalaumiana bure na kukosana bure.

Mashabiki wanaweza kumlaumu mchezaji kwa kutofunga bao ilhali wengi si wachezaji bora. Wangekuwa wachezaji bora wangekuwa uwanjani wakicheza badala ya kutazama. Utawaona wakikosoa wachezaji ilhali wenyewe wangekuwa uwanjani wangefanya makosa yayo hayo au hata zaidi. Hivyo basi naomba mashabiki wote, wasiwe wepesi wa kulaumu ilhali wenyewe ni duni hata zaidi. Tunapaswa kufahamu kuwa katika mashindano yoyote ni lazima kuwe na mshindi na mshinde. Timu yako ikishinda sawa, isiposhinda sawa. Hapana haja ya kukosana ati kwa sababu ya wachezaji ambao hata hawajui nchi ya Kenya iko katika bara gani.

Tuelewe kuwa lengo la mchezo wowote ule ni kuleta utangamano umoja na upendo. Michezo pia hukuza nidhamu baina ya wachezaji. Siku hizi wachezaji hulipwa kiasi kikubwa cha pesa . Ukweli ni kuwa uchezaji ni kazi kama ile nyingine. Tumewaona wachezaji wakijenga nyumba, kununua mashamba, kusomesha watoto na kuishi maisha ya ufanisi. Wachezaji wengi ni wafalme wanaotoa harufu ya pesa wanapopita.

---

41. Tuko na mwajificho tuko na kushi kana na kuangushana....... .Hii ni michezo gani mtawalia?
A. Miereka, kibe B. Raga, miereka
C. Kibe, Miereka D. Kodwa, gungwi

42. Yafuatayo ni sahihi kulingana na mchezo wa soka ila
A. huchezwa na wasichana
B. huchezwa na wavulana
C. huchezwa na wachezaji kumi na mmoja
D. huchezwa kwa zaidi ya dakika tisini

43. Ni kweli kuwa,
A. mchezo wa kandanda huwavutia watu wote
B. mchezo unaovutia sana ni wa kombe la dunia
C. wengi wanaohidiana si wachezaji
D. watu huwa mashabiki wa timu mbalimbali zenye jamaa zao

44. Aya ya tatu inatuonyesha kuwa
A. mchezo wa kandanda umeleta utangamano, amani na faida katika familia nyingi
B. jambo zuri linaweza kuleta athari hasi katika mshikamano wa jamaa
C. hakuna mchezo mwingine unaoweza kusambaratisha umoja wa watu kama ule wa soka
D. Si vizuri kutazama kombe la dunia katika familia ambayo inaunga mkono timu tofauti

45. Kinaya katika aya ya pili kinajitokeza pale
A. wale wanaowekeana ahadi huwa si wachezaji wa timu yoyote
B. wale wanaocheza ndio hushurutishwa kufunga bao ili mashabiki wapeana zawadi
C. wale wanaocheza huwa ndugu za wale wanaowekeana ahadi
D. familia nzima inapoamua kushabikia timu tofauti tofauti

46. Anayeongoza mchezo wa soka uwanjani ni
A. kocha
B. kochi
C. refa
D. nahodha

47. Msimamo wa mwandishi ni kuwa,
A. kama wewe si mchezaji hapana haja ya kuzua fujo timu yako ikishindwa
B. wakati umefika watu wanze kushabikia timu nyingine
C. ushindi wa timu yoyote ile ni bora kuliko furaha ya mashabiki
D. watu wawe tayari kwa matokeo yoyote yale

48. Kulingana na kifungu, mchezo
A. unaweza kuimarisha mtu kiuchumi
B. unaweza kuimarisha uhusiano wa jamii
C. unaweza kukuza vipawa vya wanariadha shupavu wa humu nchini
D. una madhara mengi kuliko faida

49. Utawaona wakikosoa wachezaji ilhali wenyewe wangekuwa uwanjani wangefanya makosa yayo hayo au hata zaidi. Ni methali gani inayoafiki kauli hii ?
A. Mcheza kwao hutuzwa
B. Kosa moja halimwachishi mke
C. Nyani haoni kundule
D. Maji yakimwagika hayazoleki

50. Wachezaji wengi ni wafalme wanaotoa harufu ya pesa wanapopita . Taja tamathali mbili zinazojitokeza katika kauli hii
A. istiara, tashbihi
B. sitiari, kinaya
C. sitiari, chuku
D. tashbihi, chuku